# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**2024**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO

**NAMBA ZA SIMU**
**Mkuu wa Shule  0654121595**
**Makamu Mkuu wa Shule.0678113707**
**Matron/Patron.0718487550**
**Shule ya Sekondari UMBA**
**S.L.P.298-LUSHOTO**
**Tarehe 24/04/2024**

## SHULE YA SEKONDARI UMBA

**Kumb.Na: USS/JI//2024/1**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………. ……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UMBA HALMASHAURI YA LUSHOTO MKOA WA TANGA MWAKA 2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya sekondari umba ipo wilaya ya LUSHOTO mkoa wa TANGA, inayo furaha kukujulisha kuwa umepangwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii, shule ni ya wavulana tahasusi za **HGL &HKL.** unapokuwa shuleni fuata sheria, kanuni na taratibu zote. shule pia ipo umbali wa kilometa 16 kutoka kituo cha mabasi MNAZI usafiri wa kutoka kituo cha mabasi hadi shuleni ni gari ndogo maarufu **Noah** nauli ni shilingi 8,000/= au usafiri wa pikipiki (**Bodaboda**) ni Shilingi 10,000/= ama kwa wale wanaotoka nje ya wilaya ya LUSHOTO au mikoani DAR-ES-SALAAM panda basi la MBUTA hadi kituo cha mabasii MNAZI, Kwa ARUSHA na KILIMANJARO panda basi la WEBA hadi kituo cha mabasi MNAZI, Kwa TANGA mjini panda basi la WEBA hadi MNAZI, Wale wanaotoka maeneo mbalimbali mbalimbali fika stendi ya Mabasi MOMBO Ulizia Gari zinazo enda MNAZI.

**MUHULA WA KWANZA WA MASOMO UTAANZA TAREHE 01 JULY, 2024.**
**HIVYO, WANAFUNZI WOTE WANAPASWA KUANZA KURIPOTI SHULENI KUANZIA TAREHE 01 JULY, 2024. SIKU YA MWISHO YA KURIPOTI ITAKUWA TAREHE 14 JULY, 2024.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

## 2.1 Sare Za Shule

Mwanao aje na:

i Suruali mbili (2) rangi Nyeusi

ii Suruali mbili (2) rangi ya ugoro

iii Shati Nyeupe Jozi mbili (2) mikono mirefu.

iv T-shirt rasmi ya Shule inapatikana Shuleni Tshs. 15,000/= (Uje nayo mkononi).

v Shuka Mbili Rangi ya bluu bahari na Blanket 1

vi Jacket jeusi, kwa ajili ya kujikinga na baridi

vii Viatu vyeusi vya ngozi, siyo buti na visiwe na visigino virefu.

viii Soksi rangi nyeupe

ix Mkanda mweusi wenye kifungio cha kawaida na sweta rangi ya bluu yenye V-shape shingoni (linapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/= aje nayo mkononi)

### 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i Jembe lenye mpini 1, panga 1, ufagio wa chelewa 1, squeezer 1.

ii Ndoo mbili za plastiki zilizo safi

iii Vyombo vya vyakula ambavyo ni sahani, kijiko na kikombe

iv Sanduku la bati size ya kati,masanduku mengine hayaruhusiwi

v Begi la darasani [school bag] na mathematical set

vi Daftari zisizopungua nane [8] counter book

vii Karatasi kwa ajili ya mitihani Rimu mbili (2)

viii Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.

ix Result slip ya Kidato cha Nne nakala itabaki kweye file.

x Picha 2 (Passport size).

xi Vitabu vya Masomo ya Tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa).

xii Uje na godoro la futi mbili na nusu

xiii SCIENTIFIC CALCULATOR KWA TAHASUSI YA HGL

## 2.3 MICHANGO MBALIMBALI

**(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA 41603100009 YENYE JINA LA UMBA SECONDARY SCHOOL)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## SHULE YA SEKONDARI UMBA

## 2.4 HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi)

Jina la mwanafunzi……………………………………………………………..........(Jina liwe sahihi na CSEE)

Tarehe ya kuzaliwa...........................… Wilaya……………….......... Mkoa……………………

(iii) Dini………………………. Dhehebu………………………………

(iv) Shule ulizosoma kabla ya kuja Sekondari ya umba

| SN | JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE MSINGI/SEKONDARI | MWAKA ULIO MALIZA |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |

**Saini ya Mwanafunzi……………………………………………………………………**

**2. MAJINA YA WAZAZI**

**a) Baba:**

Jina:.................................................................... *Yupo hai/Amefariki

Kazi:..................................................................

Dini:................................................ Dhehebu:.............................

Anwani:............................................................. Simu Namba:.......................

**b) Mama:**

Jina:.................................................................. *Yupo hai/Amefariki

Kazi:.................................................................

Dini:................................................................ Dhehebu:.............................

Anwani:.......................................................... Simu Namba:.......................

**3. Jina la atakayegharamia mahitaji ya shule**

Jina:..........................................................................

Uhusiano:............................................................... Namba ya Simu:.....................................................

# SHULE YA SEKONDARI UMBA

## 2.5 HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi)

**4. Uthibitisho wa mwanafunzi**

Mimi…………………………………………………………………….ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za Shule ya Sekondari UMBA hivyo ninakubali kwa hiari yangu, kujiunga na shule ya UMBA na kuthibitisha kuwa nitafuata Sheria na taratibu zote za shule hii, ili nitimize lengo kwa manufaa yangu/familia na taifa kwa ujumla. Endapo nitakuwa kinyume na sheria/taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa. Naahidi kutokuchelewa kurudi shuleni baada ya likizo fupi na ndefu. Saini mwanafunzi………………………………………………Tarehe……………………….

**5. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi……………………………………………………………………ninakiri kuzisoma na kuzielewa kuzielewa taratibu/sheria za shule ya sekondari umba, hivyo ninathibitisha kuwa nitatoa gharama zote za shule pamoja na mahitaji mengine, kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi aliyetajwa hapo juu asome katika mazingira mazuri kwa kipindi chote atakachokuwa hapo shuleni, kwa kuzingatia sheria na taratibu za shule ya sekondari umba aidha nathibitisha kwamba yaliyoandikwa hapo juuni sahihi. naahidi kwamba mtoto wangu hatachelewa shule kwa kukosa mahitaji (ada, michango nk)

Saini ya Mzazi/Mlezi………………………………………Tarehe………………………………

**3.**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# PO-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# UMBA SECONDARY SCHOOL
# P.O BOX 298 LUSHOTO

**Ref.No. USS/JI//01**

**To the Medical Officer**

………………………………………,

…………………………………..…..,

……………………………………….

**REF: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM**

Please, examine the student……………………………………………………………… in respect of these areas and any other area(s) deemed fit Please. Delete whichever applies.

Umba Secondary School a) Sight Yes/No. If yes, state…………………………………………

b) Hearing. Yes/ No. If yes, state ………………………………………………………...

c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes /No. If yes, state………………......................

d) Blood Pressure. Yes /No. If yes, state……….......……………………..…………

e) Any Physical Impairment(s).Yes/No. If yes, state ……………………….………………

Do you therefore recommend this student to pursue studies at this school?

………………………………………………………………………………………………..

Name………………………………………..Signature……………………..Date…………

Official Title……………………………………. Official Stamp

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**
**SHULE YA SEKONDARI** UMBA
**ORODHA YA VITABU A-LEVEL**

| | | |
|---|---|---|
| 01 | HISTORY | 1. Essentials in Advanced history paper I \|& II (Salehe Yasini).<br>2. Themes in Advanced History paper I & II (Florence M.Mavunde).<br>3.Advanced Level History Paper I & II (Zisti Kamili)<br>4.Contemporary Historical Events Advanced Level History<br>Shibitali & Son publishers ( Tumaini S.CK 2010) |
| 02 | GEOGRAPHY | 1. A comprehensive Approach to Physical Geography (D.T. Msabila).<br>2. Elementary Physical Geography: Advanced level and Colleges ( Ahmed Lubwama).<br>3.Practical Geography: Map reading, Photography and Surveying (Zisti Kamili |
| | | 1.Nadharia ya Lugha ya Kiswahili kidato cha Tano na Sita (N. Nyangwine & Masebo)<br>2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na vyuo ( Kihore, Y.M. Masamba D.P.B, TUKI<br>(2003)<br>3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: EnglishKiswahili Dictionary TUKI |
| 03 | KISWAHILI | 1. An Essential Guide paper I & II (Nicholus Asheli).<br>2. New Intergreted Advanced Level, Paper I & II (G.Mshana).<br>3. Grammar and Phonology Paper I (Michael Kadege).<br>4. Possibilities Questions and Answers Paper I & II<br>(Mgonja. H)<br>5. Oxford Dictionary |
| 04 | ENGLISH LANGUAGE | 1. General Studies for Advanced Level Certificate By Richard Mbalase (2011).<br>2. Understanding Advanced Level General Studies By Jonnes Bigirwamungu (2010).<br>3. Advanvced Level General Studies By Nyambari Nyangwine (2012). |
| 05 | GENERAL STUDIES | 1. General Studies for Advanced Level Certificate By Richard Mbalase (2011).<br>2. Understanding Advanced Level General Studies By Jonnes Bigirwamungu (2010).<br>3. Advanvced Level General Studies B |

## 3.1 HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO SHULE YA SEKONDARI UMBA SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule ya sekondari Umba ni shule ya Bweni kwa kidato cha tano na sita kwa wavulana , yenye Tahasusi za masomo ya sanaa ambazo ni HGL na HKL.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Mwanafunzi wa shule ya sekondari Umba anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi kipindi chote awapo shuleni ambayo yameorodheshwa hapo chini. Kushindwa kuzingatia na kutekeleza mwanafunzi anaweza kukosa sifa za kuendelea kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Umba na hatimaye kusimamishwa masomo ama kufukuzwa shule kabisa.

**1. SARE ZA SHULE**

1.1. Suruali nyeusi yenye marinda na isiyobana

1.2. Shati jeupe la mikono mirefu

1.3. Tracksuit rangi nyeusi

1.4. Soksi nyeupe

1.5. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

1.6. Mkanda mweusi wenye kifungio cha Kawaida

1.7. Sweta rangi ya blue

1.8. Shamba dress ni suruali ya ugoro na fulana nyeusi ya raundi

1.9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa suruali zinazobana (vimodo), vikoti, makoti, vilemba, kofia, vizibao, bangili, mkufu na mapambo kama sehemu ya sare ya shule.

10.0 Suruali mbele iwe na rinda mbili (“celebration”) kila upande na mifuko miwili ya “cross”, na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kupitisha mkanda.

11.1 Usafi wa mwili na mavazi yote yanayoruhusiwa kuvaliwa hapa shuleni ni muhimu. Ukaguzi utafanywa mara kwa mara kuthibitisha usafi huo.

**2. VIFAA VYA MICHEZO:**

2.1 Raba au viatu vyovyote vya michezo, “track suit”

**3. UVAAJI WA SARE NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE WAKATI WA:-**

3.1. Masomo darasani

3.2 Wanafunzi wanapotoka nje ya shule

3.3. Mhadhara wa Shule (BARAZA)

3.4. Maandamano ya kitaaluma

3.5. Mikutano

3.6. Mahafali (“Graduation”)

Mwanafunzi atatakiwa kuvaa shamba dress awapo katika eneo la shule nje ya muda wa vipindi vya kufundishwa Darasani na **SI VINGINEVYO.**

**4. MIPAKA YA SHULE**

4.1. Mipaka ya shule iko wazi

4.2. Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali

**4.1. WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUTEMBELEA SEHEMU ZIFUATAZO ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUMU**

4.1. Chumba maalum cha walimu (Staff room)

4.2. Ofisi za shule (school offices)

4.3. Maabara na sehemu zenye miradi ya shule

4.4. Jikoni

4.5 Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

**5. SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA**

**Ni marufuku kuonekana sehemu zifuatazo**:-

5.1. Vilabu vya pombe (Bars, Night Clubs,)

5.2. Majumba ya Starehe (Cinema Halls, Disco Halls nk)

5.3. Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses)

**6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi kipindi chote uwapo shuleni ambayo ni pamoja na.

6.1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.

6.2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa ni muhimu.

6.3. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).

6.4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

6.5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

6.6. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

6.7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.

6.8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

6.9. Kuzingatia usafi (usitupe taka/ karatasi au uchafu ovyo)

**7. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi,
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Uasherati/ubakaji/ulawiti/ushoga,
iv. Ulevi wa aina yoyote
v. Uvutaji wa sigara/bangi/utumiaji wa dawa za kulevya,

vi. Makosa ya jinai,Kupigana au kupiga,

vii. Kuharibu mali ya mtu/ umma/fedha ya serikali kwa makusudi.

viii. Kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.

ix. Kudharau bendera ya taifa/viongozi wa serikali, misafara ya viongozi wa kitaifa

x. Kuoa au kuolewa,

xi. Kupata mimba/kumpa mwanamke mimba,

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi,

xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni,

xiv. Kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule,

xv. Kutoa mimba/kushiriki katika kutoa mimba ,

xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

xvii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla,

xviii. Kufuga ndevu, mustachi au nywele ndefu pamoja kucha.,

xix. Kujipamba kwa hereni, poda, kupaka kucha rangi,

xx. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu,

xxi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.,

xxii. Kukataa adhabu kwa makusudi,

xxiii. Kutoka nje ya shule bila sare ya shule au bila kibali,

xxiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi/line ya simu/charger/Flash/memory card katika mazingira ya shule.

xxv. Kukutwa umekalia kiti ama kukitelekeza porini kwa madhumuni ya kujisomea ama vinginevyo.

xxvi. Kutumia vyombo vya umeme Bwenini/ darasani au mahali popote ndani ya Shule. Tanbihi Mwanafunzi akipatikana na Simu mzazi utalazimika pamoja na adhabu nyingine kulipia gharama za uharibifu wa miundombinu ya umeme na kumtafutia shule nyingine kijana wako [uwe tayari kumhamisha].

xxvii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**MAENEO YA KUFANYA KAZI**

**MABWENINI**

i)Kila mwanafunzi atapangiwa na mwalimu eneo la kudumu la kufanya kazi asubuhi na jioni baada ya saa za darasani.

ii) Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayeacha kuhudumia eneo lake kikamilifu. Aidha kila asubuhi/jioni mwanafunzi anatakiwa kufanya usafi katika Bweni, bwalo, eneo nk. Kama atakavyopangiwa na mwalimu/viongozi wake.

iii)Ni marufuku kuwa Bwenini wakati ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani/miradi/michezo/Roll-check/Baraza nk.

## DARASANI

Wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani

Kuanzia saa 7:45 – 10:25 asubuhi, 11:50 – 01:30 mchana, 02:10 – 3:30 Alasiri, 7:30 – 11:00 usiku.

Darasa liwe safi (lisiwe na buibui, vumbi, karatasi nk) Mwalimu wa Darasa atakagua vyumba vya madarasa mara kwa mara. Kiongozi wa darasa na kiranja wahakikishe kila darasa ni safi.

**WAKATI MWANAFUNZI AKIWA DARASANI ANATAKIWA AFANYE YAFUATAYO:-**

a) Mwanafunzi asipige kelele/asitoketoke darasani.

b) Mwanafunzi aulize na kujibu maswali

c) Mwanafunzi afanye test/mazoezi/majaribio yote kwa uwezo wake wote. Kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/test kwa kila somo.

d) Viti/madawati yapangwe kwenye mistari iliyonyooka

e) Mwanafunzi analazimika kuhudhuria vipindi vyote kwa siku.

f) “Private Study” iliyopo kwenye ratiba ya siku hiyo nilazima ifanyike darasani.

g) Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati/taa/switch n.k. kutoka darasa moja kwenda mahali pengine au Bweni moja kwenda lingine.

h) Viongozi wa wanafunzi (monita na viranja) wahakikishe kwamba hakuna kifaa kilichohamishwa kutoka darasa moja kwenda mahali bila kibali cha mwalimu wa darasa.

Pia wanafunzi wanahitajika kuhakikisha darasa linakuwa safi muda wote kushindwa kufanya hivyo sheria kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wanafunzi wa darasa husika.

**CHAKULA**

Shule inaandaa Chakula kwa ajili ya Wanafunzi wote kila Siku.Kila Mwanafunzi ni lazima ale chakula hicho kinachoandaliwa na shule. Chakula kiliwe ndani ya Bwalo ama sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya chakula, ni marufuku kupeleka chakula Bwenini au mahali pengine popote bila KIBALI maalum.

Aidha, Hakuna Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule kwa ajili ya kutafuta Chakula.

**MAELEKEZO YA LIKIZO:**

Wakati wa likizo yoyote ile NI LAZIMA mwanafunzi aondoke/ arudi nyumbani. Hivyo basi, hakikisha unampatia/ umemtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani. Shule haiwajibiki kumpatia mwanafunzi nauli, chakula na malazi wakati wa likizo.

Ni jukumu la mzazi kuona kwamba mwanafunzi wa Bweni anarudi shuleni siku angalau moja kabla ya siku ya kufunguliwa shule. Shule ikishirikiana na Bodi ya shule wana mikakati ya kuimarisha elimu ambapo mwanafunzi atakayechelewa kurudi kutoka likizo fupi au ndefu kwa wiki moja au zaidi itabidi aje na mzazi/mlezi wake. Mwanafunzi ambaye hatakuja na mzazi/mlezi hatapokelewa shuleni.

Aidha Mwanafunzi atakayechelewa siku moja hadi sita baada ya likizo fupi au ndefu atapewa adhabu kali.

Tanbihi: ukosefu wa ada kwa wanafunzi wa Bweni hautakubalika kwamba ni sababu ya kuchelewa kuja shuleni.

**MUHIMU SANA:**

Kama hukubaliani na **MASHART**I yaliyotajwa hapo juu **USIJE SHULENI** ila **MZAZI/MLEZI** atafute **UHAMISHO** wako kwenda shule nyingine. Mwanafunzi anayekuja hapa shuleni baada ya kusoma taratibu za shule hii **HATEGEMEWI KUVUNJA SHERIA/KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE** kwani akifanya hivyo ni kwa **MAKUSUDI na SIYO BAHATI MBAYA**.

**MUHIMU KWA MZAZI**

i)Mchango WOWOTE utakaotakiwa na shule ni lazima uwe na maandishi pamoja na Saini na muhuri wa Mkuu wa Shule. Kinyume cha hapo usimpe mwanao mchango ambao hauna barua.

ii)Tabia na mwenendo wa mtoto wako akiwa likizo ni JUKUMU LAKO na tutafurahi sana kama utatuandikia kuhusiana na tabia ya mtoto wako alipokuwa likizo, mema/mabaya aliyofanya, ushauri uliompa mwanao pamoja na tarehe aliyotoka nyumbani kurudi shuleni. Maelezo haya yatatusaidia sana katika malezi ya mwanao

## Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule JUMANNE S. MPILIPILI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

Headmaster
Umba Secondary School
P. O. Box 298, Lushoto

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0654-121-595**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0678-113-707**
- **Mwandamizi Taaluma 0658-060-952**
- **Mwandamizi Malezi 0718-487-550**